# Mbinu za Utunzi wa Nyimbo za Uganga wa Pepo Zanzibar: Mifano kutoka Jamii ya Watumbatu

Hassan Gora Haji

## Ikisiri

Miongoni mwa amali za kijadi za Wazanzibari ni uganga wa pepo (uganga wa shetani). Katika kila kijiji cha Zanzibar hakosekani mganga wa asili. Mganga huyo anaweza kuwa wa mitishamba, mahirizi, makafara, zinguo au pungwa kama *komero*, *rubamba*, *puuwo* na *umundi*. Katika makala hii tunazungumzia mtindo wa nyimbo za uganga wa pepo – mbinu za utunzi (nyimbo hizi hutungwaje?) hususan katika jamii ya Watumbatu. Waganga wa pepo mara nyingi hutumia nyimbo wakati wa kupunga ili kunogesha uganga na kurahisisha pepo wa muwele apande kichwani kwa haraka kwani inadhaniwa kuwa pepo nao pia wanapenda muziki na nyimbo. Kwa hivyo, wanapoimbiwa hupanda kichwani mara moja bila ya kuchelewa. Nyimbo za uganga wa pepo zimegawanyika katika makundi mawili: nyimbo zinazofuata kaida za ushairi wa kimapokeo, na nyimbo zisizofuata kaida za arudhi. Mara nyingine nyimbo za uganga wa pepo huimbwa kufuatana na matukio ya uganga wenyewe unavyofanywa. Makala hii basi inalenga kuzichunguza nyimbo hizo hususani mbinu zake za utunzi. Utafiti wetu umebaini kuwa nyimbo hizo hutumia mbinu mbalimbali katika utunzi wake.

## 1.0 Utangulizi

Uganga wa pepo ni asasi ya jadi ya matibabu ambapo mara nyingi unapofanywa waganga hutumia nyimbo wakati wa kumwita pepo au shetani kutoka kwa muwele. Uganga huu upo wa aina nyingi kutegemea aina ya pepo au ngoma ya pepo inayotumika kupungia. Tukiangalia kigezo cha aina ya ngoma tunapata aina za uganga wa *komero*, uganga wa *puuwo*, uganga wa *umundi*, uganga wa *mchanja*, uganga wa *rubamba*, uganga wa *tari* au *kitari*, uganga wa *kibuhudadi*, uganga wa *koikoi*, uganga wa *pungwa* na uganga wa *kumbwaya*. Lakini tukichukua kigezo cha aina ya pepo tunapata uganga wa *maruhani*, uganga wa *kibuki*, uganga wa *rubamba* (hii pia ni ngoma) na uganga wa *puuwo* (hii pia ni ngoma). Lengo la makala hii ni kubainisha na kuchambua mbinu mbalimbali zinazotumika katika utungaji wa nyimbo za uganga wa pepo visiwani Zanzibar. Utafiti huu umefanywa katika vijiji vya Chaani, Kiwengwa, Mkwajuni na Tumbatu Kichangani katika Mkoa wa Kaskazini, Unguja Zanzibar mwaka 2011 hadi 2015. Katika maeneo haya hasa wanatumia lahaja ya Kitumbatu kwani kwa ujumla, wakaazi wa Mkoa wa Kaskazini Unguja ni Watumbatu. Katika kufanya utafiti huu tulitumia mbinu za umakinifu (ushuhudiaji) na mahojiano ya ana kwa ana kati ya mtafiti na waganga wa *pungwa* na wari wa zamani (watu waliowahi kupungwa). Katika Mkoa wa Kaskazini Unguja ambako utafiti huu ulifanywa kuna uganga wa pepo wa aina kuu mbili: uganga wa *maruhani* na uganga wa *puuwo*. Uganga wa maruhani

unajumuisha uganga wa *komero, kibuhudadi* na *kitari,* na ule wa *puuwo* unajumuisha uganga wa *mchanja*, pungwa na *rubamba*.

Kwa mujibu wa watoa taarifa wetu ambao ni Ali Kombo na Mwajuma Ali, wakaazi wa Chaani-Unguja, inasadikiwa kuwa nguvu na uwezo wa pepo upo katika kulinda mashamba, mali, miji, na mitaa; na pepo hao wapo wa aina nyingi na wana majina yao. Kwa mfano, Mwana-wa-Mwana, Simba, Kalibi Kasi, Mwajuma Kirobo, Fungua Lango, Funga Nangwe, Mapara, Mpaji Kani, Ame Mkuwi, Chacha Nangwe, Mkozingo, Fundi Yuni, na Gora Kipepo. Majina haya ya pepo yanapatikana kaskazini Unguja pamoja na kisiwa cha Tumbatu. Aina nyingine ya pepo ni pamoja na Kitimiri, Nyange, na Mrewa (taz. Alpers, 1984).

Makala hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu; utangulizi, mjadala na hitimisho. Katika sehemu ya utangulizi tunafafanua dhana ya mtindo kwa mujibu wa wataalamu. Sehemu hii inafuatiwa na sehemu ya uchambuzi wa mbinu za utunzi wa nyimbo hizo kama vile maneno ya kiganga, lugha za kigeni na lahaja, matumizi ya arudhi, matumizi ya takriri, lugha ya picha na ishara, misemo na tamathali za usemi. Sehemu hii inafuatiwa na hitimisho pamoja na mapendekezo ya mwandishi juu ya kuendeleza utafiti wa nyimbo za uganga wa pepo. Nyimbo zote zilizotumika katika makala hii zimekusanywa na kutafsiriwa na mwandishi wa makala hii.

Mbinu ni kipengele kimojawapo cha mtindo katika kazi ya fasihi, ambapo kuna mbinu za utunzi na mbinu za utendaji. Mbinu za utunzi hujumuisha vipengele vya matumizi ya lugha, mbinu za kiuandishi na matumizi ya picha na ishara. Msokile (1992) na Madumulla (2009) wanakubaliana kuwa mtindo: a) unaweza kuwa ni mchangamano wa mambo mawili ambayo ni: i) wazo la msanii na jinsi wazo hilo linavyoelezwa, na ii) msanii na kazi yake anavyoiwasilisha; b) unaweza kuwa ni tabia ya uandishi katika kipindi cha mfumo fulani wa maisha au historia, na c) unaweza kuwa ni tabia ya mtu binafsi ya ufundi, umahiri na hisia za kibinafsi katika kutenda mambo yake. Lakini Nkwera (ht.) anaeleza kuwa ziko nyimbo zenye beti chache tu, zenye viitikio, zinazofuata arudhi (zenye urari wa vina na mizani) na pia zipo nyimbo huru (nyimbo zisizofuata arudhi) (uk. 55). Tukichunguza kwa makini maelezo haya ya Nkwera tunagundua kuwa ingawa anazungumzia aina za nyimbo lakini pia anagusia mbinu zinazotumika kutungia nyimbo hizo. Hivyo mbinu hizi kama vile vina, mizani, mpangilio na idadi ya beti, mishororo, muwala na kujitosheleza ni sehemu ya mtindo. Naye, Rashid (2008) anabainisha mitindo kadhaa ya nyimbo za Kiswahili kama vile takriri neno, takriri mshororo, matumizi ya vina vya kati na vya mwisho, kufanana au kutofautiana, na takriri ya mkarara/ kiitikio cha wimbo.

Finnegan (1970) anaeleza kuwa nyimbo nyingi za asili hutumia mbinu ya takriri na majibizano kati ya mwimbaji na waitikiaji. Pia, anasema kuwa katika uimbaji, mwisho wa nyimbo hizo kwa kawaida huwa haufahamiki vyema. Wakati

mwingine katika baadhi ya nyimbo za asili, mwimbaji hupokewa kuimba na waitikiaji wake au hupokewa na ala za muziki (kur. 259-261). Kwa maana hiyo, tunaweza kueleza kuwa mtindo ni kipengele kimojawapo cha fani katika kazi ya fasihi. Mtindo katika kazi ya fasihi ndio unaojumuisha vipengele vya mbinu za utungaji na uwasilishaji au utendaji. Katika sehemu inayofuata tunaelezea mbinu hizo za utungaji wa nyimbo za uganga wa pepo Zanzibar.

## 2.0 Mbinu za Utunzi wa Nyimbo za Uganga wa Pepo

Utafiti huu umebaini kuwa kufuatana na hatua za kufanya uganga wa pepo, nyimbo hizo zimegawanyika katika makundi kadhaa ambayo ni: nyimbo za kuanzia uganga, nyimbo za kuchombezea, nyimbo za kushajiiisha au kuhamasisha, nyimbo zinazoimbwa wakati pepo anapokuja kichwani mwa mwari mpungwa, nyimbo za kufurahia baada ya kuja pepo, nyimbo za wakati wa kutoa salamu na jina, nyimbo za wakati wa kulipwa pepo kilemba au chano na nyimbo za kumalizia uganga. Hivyo basi, kwa kila mfano wa wimbo tunaoutumia tunaonesha pia wimbo huo upo katika kundi gani. Mbinu za utungaji tunazojadili katika makala hii ni matumizi ya maneno ya kiganga, lugha za kigeni, lahaja, arudhi, takriri, lugha ya picha na ishara, misemo na matumizi ya tamathali za semi:

### 2.1 Matumizi ya Maneno ya Kiganga, Lugha za Kigeni na Lahaja

Katika utungaji wa nyimbo za uganga, maneno ya kiganga na yenye asili ya Kiarabu au dini ya Kiislamu, na maneno ya lahaja za Kitumbatu na Kipemba yametumiwa.

#### 2.1.1 Matumizi ya Maneno ya Kiganga

Katika nyimbo za uganga zilizokusanywa mtafiti amegundua kuwa kuna msamiati wa kiganga uliotumika katika nyimbo za uganga wa *komero* (uganga wa maruhani) na ule wa *puuwo* (uganga wa jini mweusi). Kwa mfano, katika nyimbo tulizoziwasilisha hapa chini maneno kadhaa yametumika; maneno hayo ni pamoja na *kombe.* Kombe ni aina ya dawa ya kunywa inayotokana ya maandishi ya Kiarabu (BAKIZA, 2010). Mganga huandika baadhi ya aya za Kur-an kwa zafarani au masinzi katika sahani nyeupe au katika kuti la mnazi kisha hufutwa kwa maji safi na kutiwa chupani. Mgonjwa hunywa na kujipaka mwilini mwake kwa kiasi atakachoelekezwa na mganga. Neno hili linatumika katika uganga wa maruhani sio katika uganga wa *puuwo*. Katika uganga wa *puuwo* hutumika *jimbo* (dawa ya mchanganyiko wa majani ya miti mbalimbali inayotoa harufu mbaya) badala ya kombe. Neno jingine ni *gamela* (chano), ambalo maana yake ni jumla ya vyakula anavyopewa shetani au pepo kupitia kwa mwari au muwele kama malipo au fidia ya kumuachia mgonjwa. *Chano* ni pamoja na mkate wa kumimina (mkate wa mchele), halua, tende, muwa, asali, yungiyungi (jeupe kwa maruhani na jeusi kwa

pepo wa *puuwo*), sharubati na vidole vichache vya ndizi mbivu ya pukusa. Neno *yungi* ambalo ni ufupisho wa yungiyungi, pia hutumika katika nyimbo hizi. Yungi ni aina ya ua la mmea wa myungiyungi unaoota katika maji baridi ya mto au ziwa. Kuna aina mbili za mayungiyungi: meupe na meusi. Kwa shetani wa maruhani hutumika yungiyungi jeupe na kwa shetani/pepo wa puuwo hutumika yungiyungi jeusi. Nyimbo hizi za uganga pia hutumia neno *uzari* kumaanisha kilemba anachopewa mtu aliyepungwa kama fidia au malipo ya shetani au pepo. Kwa pepo au shetani wa komero au maruhani ni kitambaa cheupe chenye urefu wa mita nne na kwa shetani wa *puuwo* ni kitambaa chekundu cha aina ya bafta. Neno jingine ni *kiringe* ambalo humaanisha asili/jadi ya uganga wa pepo/shetani au pahala panapofanywa uganga wa pepo/shetani au ni tendo la kubabaishababaisha. Hivyo basi, maneno haya (ambayo katika nyimbo tumeyakoleza wino) hutumiwa na waganga katika shughuli zao za uganga tu na katika utunzi wa nyimbo zao. Nyimbo zifuatazo zinadhihirisha matumizi ya istilahi hizo za uganga wa pepo. Nyimbo hizi, zipo katika lahaja ya Kitumbatu na mwimbaji (mganga) wa nyimbo hizi; Bwana Ussi Makame Nyange ni Mtumbatu.

**Nyimbo katika Kitumbatu**

**Nakwita Kweli**
(wimbo wa wakati anapotaka kuja pepo)
1. *Nakwita kweli miye x 2,*
2. *Kuna **gamela** na njiwa,*
3. *Kweli si urongo,*
4. *Nakwita kweli miye.*
5. *Mnajampa nini we,*
6. *Mnakuja rijali ee,*
7. *Mnakuja?*

**Nataka Yungi**
(wimbo uimbwao anapolipwa pepo kilemba/chano)
1. *Nataka **yungi** na njiwa,*
2. *Na **hanamu** yangu hapandia.*
3. *Nipokwisha hapima **uzari** wangu, hogelea.*
4. *Nassoro we Nassoro, twii kahawa,*
5. *Ugovi wa **kiringe** mbaya.*
6. *Ooh hogelea,*
7. *Ooh oh hogelea.*

**Tafsiri kwa Kiswahili**

**Ninakwita Kweli**
1. Ninakwita kweli mimi x 2,
2. Kuna chakula cha pepo na njiwa,
3. Kweli si uongo,
4. Ninakwita kweli mimi,
5. Mtakujampa nini we,
6. Anayekuja rijali ee,
7. Anayekuja?

**Nataka Yungiyungi**
1. Ninataka yungiyungi na njiwa,
2. Na mnyama wangu nikapandia.
3. Nilipokwisha nikapima kilemba changu, nikaogelea,
4. Nassoro we Nassoro nipe kahawa
5. Ugomvi wa ugangani mbaya
6. Ooh huogelea,
7. Ooh huogelea.

### 2.1.2 Matumizi ya Maneno yenye Asili ya Kiarabu au Dini ya Kiislamu

Vilevile watunzi wa nyimbo za uganga wa pepo wanatumia baadhi ya meneno yenye asili ya Kiarabu na dini ya Kiislamu. Hii inatokana na kuaminika kuwa pepo au shetani hasa wa maruhani (wale wa komero) ni waumini wa dini ya Kiislamu na wengi wao wana asili ya Uarabuni. Kwa maana hiyo, watunzi hutumia maneno

hayo kuonesha uasili wa shetani au pepo na kuwavutia au kuwafurahisha hao pepo na kuwafanya wapande kichwani kwa haraka. Maneno hayo yaliyotumika katika utungaji wa nyimbo ni pamoja na: *jini* – kiumbe kisichoonekana kwa macho na kimeumbwa kwa moto (BAKIZA, 2010), *ijilisu* – kaa/keti, *fil* – katika/ndani, *bismillahi* – naanza kwa jina la Mwenyezi Mungu, sheilula[1], *hewallah/hewala*[2] – sawa/nakubali, *yamilikitabu* – katika kitabu. Nyimbo zifuatazo za uganga wa maruhani zinabainisha maneno hayo:

| Nyimbo katika Kitumbatu | Tafsiri kwa Kiswahili |
|---|---|
| **Bismillahi ya Milikitabu**<br>(wimbo wa kufurahia kuja kwa pepo) | **Ninaanza kwa Jina la Mwenyezi Mungu katika Kitabu** |
| 1. ***Bismillahi ya milikitabu*** *x2,* | |
| 2. *Yamilikitaaa, ya milikitabu.* | 1. Bismillahi katika kitabu x2, |
| 3. ***Hewalla*** *baba ya milikitabu,* | 2. Katika kitabu, katika kitabu. |
| 4. *Yamilikita ee ya milikitabu.* | 3. Nakubali baba katika kitabu, |
| 5. *Bismillahi ya milikitabu,* | 4. Katika kitabu, katika kitabu. |
| 6. *Hewalla baba ya milikitabu.* | 5. Bismillahi katika kitabu, |
| | 6. Nakubali baba katika kitabu. |

| | |
|---|---|
| **Sheilula**<br>(wimbo wa kuanzia uganga) | **Tafadhali** |
| 1. ***Sheilula*** *wee x2, jini wa jinani,* | 1. Shekhe wa Allah wee x2, jini wa jinani, |
| 2. ***Ijilisu*** *x2* ***fili makani*** *wee,* | 2. Kaa x2 katika makazi wee, |
| 3. *Salia Manga wee ee, kaumu ruhani.* | 3. Bakieni nyote Umangani we ee, wafuasi wa majini. |

Maneno ya Kiarabu au ya kidini ya Kiislamu yanajitokeza zaidi katika nyimbo za uganga wa komero kwa sababu uganga huo unajishughulisha na kutibu wagonjwa waliodhuriwa na pepo/shetani wa maruhani ambaye anasadikiwa ni mcha Mungu asiyependa kufanya au kufanyiwa mambo mabaya. Kauli hii ya ucha Mungu inathibishwa katika Kur-an Tukufu kuwa binadamu na majini yameumbwa na Mwenyenzi Mungu ili kumuabudu Yeye tu. Katika Kur-an Tukufu, sura ya hamsini na moja (Adh-dhaariyaat), aya ya hamsini na sita inasema:

*Sikuwaumba majini na watu ila wapate kuniabudu* (51: 56).

---

[1] Neno hili linatokana na maneno mawili ya Kiarabu: Sheikh na Lillah. Kwa maana hiyo, maneno haya yakiwekwa pamoja yanakuwa na maana ya shehe wa Mwenyezi Mungu. Neno hili pia linapatikana katika kasida ya zikri ya kadiria ambayo maneno yake yanasema hivi: Lailahailallah Muhammad Rasulu Allah, Abdul-kadri sheilullah. Sheilula ni neno la kiganga linalotumiwa kumuomba pepo au shetani atulie baada ya kuja kichwani mwa muwele. Pia hutumiwa kumuomba pepo apande au aje kichwani mwa muwele kwa haraka bila ya matatizo na kuchelewa.

[2] Hili ni tamko la kuridhia jambo aliloambiwa mtu (BAKITA, 2010: 115) ikimaanisha ni sawa au kukubaliana na jambo hilo aliloambiwa. Katika muktadha wa kiganga pia limetumiwa kwa maana hiyohiyo.

Pepo wa maruhani ni muumini wa dini ya Kiislamu na ndiyo maana waganga, watunzi na waimbaji wa nyimbo za uganga wa komero hutumia maneno hayo ya kidini au Kiarabu. Na hii ndiyo tofauti mojawapo kati ya nyimbo za komero na zile za puuwo.

### 2.1.3 Matumizi ya Lahaja

Maneno mengi yaliyotumiwa katika nyimbo za uganga wa pepo zilizochambuliwa katika makala hii yametokana na lahaja za Kitumbatu na mengine machache yametoka katika lahaja ya Kipemba (taz. 2.1.3.2). Kitumbatu ni miongoni mwa lahaja za Kiswahili zinazozungumzwa Zanzibar. Kitumbatu huzungumzwa na Waswahili wa kisiwa cha Tumbatu za sehemu nyingine za Mkoa wa Kaskazini Unguja. Na Kipemba ni lahaja inayozungumzwa na Waswahili wa kisiwa cha Pemba, Zanzibar. Katika makala hii, ingawa lahaja ya Kipemba imetumika katika baadhi ya nyimbo, hii haimaanishi kwamba utafiti huu ulifanyika Pemba.

#### 2.1.3.1 Matumizi ya Maneno ya Lahaja ya Kitumbatu

Nyimbo nyingi za uganga wa pepo tulizokusanya zina matumizi makubwa ya maneno ya lahaja ya Kitumbatu lakini hapa tunabainisha machache tu kama mfano. Matumizi makubwa ya maneno hayo yanadhihirisha asili ya uganga wa pepo, hasa uganga wa komero (uganga wa maruhani) kuwa ulianza katika kisiwa cha Tumbatu. Hii ni kwa mujibu wa mahojiano na mganga wa komero, Mzee Ali Kombo Gora tarehe 14 na 17/01/2011. Maneno ya Kitumbatu yaliyotumika katika kutunga nyimbo hizo ni kama: *nendele* (niendee), *kuwa* (kuna) *mnajampa* (mnakujampa), *mnakuja* (anayekuja), *yuno* (huyu) na *sasema* (nitasema). Nyimbo zifuatazo zinadhihirisha matumizi hayo ya maneno ya Kitumbatu:

| **Nyimbo katika Kitumbatu** | **Tafsiri kwa Kiswahili** |
|---|---|
| **Gide na Wamanga** | **Jiddah na Wamanga** |
| (wimbo wa kushajihisha/kuhamasisha) | |
| 1. *Gide na Wamanga, Gide x2.* | 1. Jiddah na Wamanga, Jide x2 |
| 2. *Kule nitokako* ***kuwa*** *jabali jeupe,* | 2. Kule nitokako kuna jabali jeupe |
| 3. *Na Wamanga majini* ***wasaliako.*** | 3. Na Wamanga majini wanakobakia |
| 4. *Kule ee,* | 4. Kule ee, |
| 5. *Kule Manga.* | 5. Kule Manga. |
| 6. *Kule ee,* | 6. Kule ee, |
| 7. *Kule Manga.* | 7. Kule Manga. |
| 8. *Mali ya shei x2,* | 8. Kitu chochote x2 |
| 9. *Na Wamanga x2.* | 9. Na Wamanga x2 |
| 10. *Nipeni upanga* ***nendele*** *Gide,* | 10. Nipeni upanga niendee Jide |
| 11. *Na Wamanga.* | 11. Na Wamanga, |
| 12. *Mali ya shei na Wamanga.* | 12. Kitu chochote na Wamanga. |

| **Jini Wenu** | **Jini Wenu** |
|---|---|
| (wimbo wa kufurahia kuja pepo) | |
| 1. ***Yuno** jini wenu wa kipembe **sasema** naye,* | 1. Huyu jini wenu wa kipembe nitasema na yeye, |
| 2. *Yuno jini anataka ng'ombe wala hanaye.* | 2. Huyu jini anataka ng'ombe wala hana. |

Sababu ya kutumika maneno hayo ya lahaja ya Kitumbatu, mbali ya kuonesha asili ya uganga wa komero kuwa Tumbatu, watunzi au waganga tuliowahoji asili yao ni Tumbatu pia. Hivyo wanazungumza lahaja hiyo huku wakichanganya na Kiswahili sanifu kutokana na maingiliano ya watu na kujifunza Kiswahili sanifu katika skuli.

#### 2.1.3.2 Matumizi ya Maneno ya Lahaja ya Kipemba

Utafiti huu umebaini kuwa baadhi ya nyimbo za uganga zina matumizi ya lahaja ya Kipemba, ingawa si kwa kiasi kikubwa, hususani katika nyimbo za uganga wa puuwo ambao unasadikiwa kuwa asili yake ni kisiwa cha Pemba. Kwa hivyo, matumizi haya yanaonesha athari za uasili wa uganga huu wa puuwo. Maneno hayo yaliyo katika uganga wa puuwo ni kama vile *nombe* (niombe), *nombere* (niombee), *usambe* (usidhani), *mwandanganya* (mnanidanganya), kama yanavyojitokeza katika nyimbo zifuatazo:

| **Nyimbo katika Kipemba** | **Tafsiri kwa Kiswahili** |
|---|---|
| **Nombe** | **Niombe** |
| (wimbo wa kuanzia uganga) | |
| 1. ***Nombe** x2,* | 1. Niombe x2, |
| 2. *Nombe, **nombere** Mungu,* | 2. Niombe, niombee Mungu, |
| 3. *Nombe na waganga.* | 3. Niombe na waganga. |
| 4. *Kuomba tushaomba,* | 4. Kuomba tumeshaomba, |
| 5. *Kuwa wee,* | 5. Kuwa wee, |
| 6. *Kuwa kwa Mungu,* | 6. Kuwa kwa Mungu, |
| 7. *Kuwa.* | 7. Kuwa. |
| | |
| **Usambe** | **Usidhani** |
| (wimbo wa kufurahia kuja pepo) | |
| *1. Usambe, usambe,* | 1. Usidhani, usidhani, |
| 2. *Watoto mwandanganya.* | 2. Watoto mnanidanganya. |

Tofauti mojawapo ya nyimbo za uganga wa *komero* na zile za uganga wa puuwo ni kwamba *komero* hutumia Kitumbatu na *puuwo* hutumia Kipemba.

### 2.2 Matumizi ya Arudhi

Arudhi ni kanuni ya utunzi wa ushairi (BAKITA, 2010: 11). Kanuni hii hasa inahusu utunzi wa ushairi wa kimapokeo ambao unajumuisha vipengele vya vina,

mizani, mpangilio maalumu wa idadi ya beti na mishororo ya kila ubeti wa shairi, utenzi au wimbo na kadhalika.

### 2.2.1 Matumizi ya Vina na Mizani

Vina ni silabi zenye milio inayofanana (Mulokozi, 1996: 100) ambazo huwekwa katikati au mwishoni mwa kila mshororo wa ubeti wa wimbo au shairi au utenzi. Nyimbo za asili za Kiswahili kama hizi za uganga wa pepo hazina ulazima wa kuwa na vina na ikitokea kuwa na vina pia sio lazima vina hivyo vitokee katikati na mwisho; mara nyingi hutokea mwishoni mwa kila mshororo wa wimbo kama tunavyoona katika makala hii. Katika nyimbo ambazo tumekusanya katika utafiti huu vina vinavyojitokeza katika nyimbo za uganga wa maruhani ni vya mwisho tu. Kwa mfano, katika wimbo ufuatao wa ‘Sina Hailipi Deni’ una kina cha mwisho -ni kama ifuatavyo:

**Sina Hailipi deni**

(wimbo unaoimbwa wakati pepo anapolipwa kilemba/chano)

1. *Sina hailipi x2 de**ni**,*
2. *Ujanja wa deni kulipa kwa mwana wa maji**ni**,*
3. *Sina hailipi de**ni**.*

Mulokozi (1996: 100) anasema kuwa kazi ya vina ni kuongeza mvuto wa mlio wa shairi, kumalizia mistari au vipande, kusisitiza maudhui na kurahisisha uhifadhi wa mashairi kichwani. Pia, vina ni moja ya mbinu zinazotumiwa na washairi ili kuleta muwala wa urari wa sauti ambazo husababisha wizani (mapigo ya kimuziki) ambao humfanya msikilizaji kuvutiwa na kunata katika wimbo.

Kwa upande wa mizani, nyimbo za uganga zilizokusanywa katika utafiti huu kwa kiasi kikubwa hazina urari wa mizani katika mishororo yake. Hapa ni vema tukaelewa kuwa wimbo ni miongoni mwa bahari za ushairi, na ushairi una sifa zake bainifu. Baadhi ya sifa hizo ni wizani (mapigo ya kimuziki), iktisadi ya maneno (matumizi ya maneno machache), matumizi ya lugha ya picha na ishara na takriri ya sauti (irabu au konsonanti), takriri neno na mshororo. Sifa moja kubwa ya wimbo ni kuimbika lakini shairi si lazima liimbike. Hoja yetu ni kinyume na alivyosema Abedi (1954) kuwa shairi kama haliimbiki halina maana. Kinacholifanya shairi liimbike ni wizani, mpangilio mzuri wa maneno, takriri ya sauti, maneno na mishororo pamoja na mjumuisho wa muziki wa ala, kama anavyosema Mulokozi (1996) kuwa baadhi ya fani za ushairi huambatana na muziki wa ala na wakati mwingine hupata wizani wake kutokana na mapigo ya muziki huo wa ala. Maana, hisia na hali ya kishairi hutokana na mwingiliano huo wa maneno, sauti na vitendo vya mtambaji na mazingira ya utendaji. Kazi kubwa ya mizani ni kuleta urari wa mapigo ya kimuziki katika masikio ya msikilizaji na pili kuliwezesha shairi kuimbika. Lakini wimbo waweza kuimbika bila ya kuwapo

urari huo wa mizani kama nilivyokwishakueleza hapo kabla. Mathalani, mshororo wa kwanza wa wimbo wa 'Ukarara' hapa chini una mizani 12 na unaishia na silabi -ka, wa pili una mizani 16 na unaishia na silabi –ma, na wa tatu una mizani 13 na unaishia na silabi -ma. Pia, wimbo wa 'Mwana wa Mganga' hauna urari wa mizani wala vina. Mshororo wa kwanza una mizani 8 na unaishia na silabi -nga na mshororo wa pili una mizani 9 na unaishia na silabi -wa. Kwa hiyo, tunaona kuwa nyimbo hizi hazikufuata mbinu ya matumizi ya urari wa mizani na vina kama zinavyonekana hapa chini:

| **Nyimbo katika Kitumbatu** | **Tafsiri kwa Kiswahili** |
|---|---|
| **Ukarara** | **Ukarara** |
| (wimbo uimbwao wakati pepo anapotoa salamu/chano) | |
| 1. *U/ka/ra/ra/ we/zi/o wa/na/ku/che/ka x2,*<br>*1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12* | 1. Ukarara wenzio wanakucheka x2, |
| 2. *U/ka/ra/ra/ wa/chu/ku/a/ ki/bu/yu, / we/nda/ ku/ge/ma.*<br>*1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16* | 2. Ukarara unachukua kibuyu, unakwenda kugema. |
| 3. *Mu/o/ngo/ u/yo, / m/ge/ni/ ha/che/zi/ ngo/ma.*<br>*1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13* | 3. Mwongo huyo, mgeni hachezi ngoma. |
| **Mwana wa Mganga** | **Mtoto wa Mganga** |
| (wimbo wa kuanzia uganga) | |
| 1. *Mwa/na/ wa/ m/ga/nga/ ha/nga x2,*<br>*1 2 3 4 5 6 7 8* | 1. Mtoto wa mganga hangi x2, |
| 2. *Mwa/na/ wa/ m/ga/nga/ hwa/ngi/wa.*<br>*1 2 3 4 5 6 7 8 9* | 2. Mwana wa mganga huangiwa. |

Hali hii inadhihirisha kuwa asili ya nyimbo za Kiswahili (kama za ngoma, uganga, jando, harusi n.k.) si urari wa vina na mizani. Kuhusiana na ushairi wa Kiswahili, Senkoro (1988: 10) anashadidia pia kwamba "kwa sababu tunajua wazi kuwa historia ya ushairi wa Kiswahili haianzi na matumizi ya vina na mizani – kwani tuna ushairi mwingi wa Kiswahili kutoka katika fasihi simulizi ambao haufuati 'sheria' za vina na mizani". Aidha, Senkoro (1998) anaeleza kuwa sio lazima kuwapo na vina katika shairi ili kuleta wizani (mapigo ya kimuziki) kama nilivyotangulia kusema hapo kabla. Nao Mulokozi na Kahigi (1979: 11) wanaeleza kuwa mtindo usiofuata vina na urari wa mizani ni wa kijadi katika fasihi ya Kiswahili na Kibantu. Mtindo wa vina na urari wa mizani umekuja baadaye kabisa (taz. pia Haji, 2011).

### 2.2.2 Matumizi ya Mishororo

Mishororo ni mistari ya ubeti wa wimbo au shairi. Nyimbo za uganga zilizokusanywa katika utafiti huu zina idadi tofauti ya mishororo. Mathalani, zipo

nyimbo zenye mshororo mmoja tu kama vile wimbo ufuatao wa uganga wa puuwo uitwao 'Lemba' ambao huimbwa pepo anapolipwa kilemba:

| **Wimbo katika Kitumbatu** | **Tafsiri kwa Kiswahili** |
|---|---|
| *Lemba langu, linang'ara kama ngao.* | Kilemba changu kinang'ara kama ngao. |

Pia kuna nyimbo ambazo zimetungwa kwa mishororo miwili. Kwa mfano, wimbo ufuatao wa uganga wa puuwo uitwao 'Mwana wa Mganga' huimbwa wakati wa kuanzia uganga (Haji, 2011):

| **Wimbo kwa Kitumbatu** | **Tafsiri kwa Kiswahili** |
|---|---|
| 1. *Mwana wa mganga hanga x2,* | 1. Mtoto wa mganga hakwangi, |
| 2. *Mwana wa mganga hwangiwa.* | 2. Mtoto wa mganga hukwangiwa. |

Pia, kuna nyimbo ambazo zina ubeti wenye mishororo mitatu kama vile 'Sheilula' (kama tuliyoona hapo awali) na 'Nyuki' hapa chini:

| **Wimbo katika Kitumbatu** | **Tafsiri kwa Kiswahili** |
|---|---|
| **Nyuki** | **Nyuki** |
| (wimbo wa kuchombezea) | |
| 1. *Nyoki wenda mbio x2.* | 1. Nyuki wanakwenda mbio, |
| 2. *Keshalikanyaga jiwe la msio,* | 2. Ameshalikanyaga jiwe la msio,[3] |
| 3. *Nyoki wenda mbio.* | 3. Nyuki wanakwenda mbio. |

Kwa ujumla, nyimbo za uganga zilizokusanywa katika utafiti huu zina beti zenye idadi tofautitofauti ya mishororo. Kuna zenye mshororo mmoja, miwili, mitatu au minne. Kwa kiasi kikubwa nyimbo za uganga wa komero (maruhani) na zile za puuwo ni fupifupi; hazizidi beti mbili. Nyimbo hizi zinakuwa fupifupi kwa sababu ya kuwa na dhamira moja. Kwa hivyo, dhamira moja haihitaji beti na mishororo mingi kuiwasilisha. Hali hii ya ufupi pia husababisha wimbo kuwa na muondoko wa harakaharaka, yaani muziki na wimbo huimbwa harakaharaka.

## 2.3 Matumizi ya Takriri

Msokile (1992: 61) anaeleza kuwa takriri ni urudiaji wa maneno, silabi au sauti zinazolingana katika kazi ya sanaa. Kwa kiwango kikubwa nyimbo za uganga wa pepo zinatumia mbinu ya takriri, mathalani takriri neno na takriri mshororo. Kutokana na muundo wa nyimbo hizi za uganga wa pepo kuwa fupifupi mtunzi hurudiarudia maneno mara nyingi ili kupata mapigo ya sauti yanayofanana na kuleta mvuto fulani kwa wasikilizaji na mwari mpungwa pale zinapoimbwa pia. Kwa mfano, katika wimbo 'Nombe' neno *nombe* limerudiwa mara 4, katika wimbo 'Gide na Wamanga'; neno *kule* limerudiwa mara 4, na katika wimbo

[3] Jiwe la kusagia liwa.

'Nakwita Kweli' neno *kweli* limerudiwa mara 3 (nyimbo hizi zote tumezielezea katika kurasa za huko juu). Pia, kuna nyimbo ambazo zimetungwa kwa kurudiwarudiwa mishororo yake kama wimbo 'Kimanga' hapa chini unavyoonesha:

| **Wimbo katika Kitumbatu** | **Tafsiri kwa Kiswahili** |
|---|---|
| **Kimanga** | **Kimanga** |
| 1. *Kimanga we, kimanga,* | 1. Kimanga we, kimanga, |
| 2. *Mwacheni aruke kimanga.* | 2. Mwacheni aruke kimanga. |
| 3. *Shurushuru Mmanga kwa upanga,* | 3. Churuchuru Mmanga kwa upanga, |
| 4. *Mwacheni aruke kimanga,* | 4. Mwacheni aruke kimanga, |
| 5. *Shurushuru upanga kwa upanga*. | 5. Churuchuru upanga kwa upanga. |

Katika wimbo huu mshororo *mwacheni aruke kimanga* umerudiwa mara mbili na mshororo *shurushuru mmanga kwa upanga* nao unarudiwa ila unaporudiwa neno 'Mmanga' linabadilishwa na kuwa upanga lakini silabi inayomalizia maneno hayo ni ileile ya *–**nga***. Hali hii inaleta mapigo ya kimuziki na mvuto na kusaidia kusisitiza maudhui husika vizuri.

## 2.4 Matumizi ya Lugha ya Picha na Ishara

Msokile (1992: 61) anaeleza kuwa picha ama taswira ni kiwakilisho cha kitu kwa maneno au kitu halisi, na kiwakilisho hicho kinaweza kufahamika kwa mtu mmoja au watu wengi zaidi. Kimaandishi, kiwakilisho hicho kinapambanuliwa kwa matumizi mazuri ya lugha. Picha za kisanaa zinajitokeza kwa misingi kuwa vitu vinavyowakilishwa kipicha vinafahamika. Kwa msingi huo, picha ni kitambulisho maalumu cha lugha ya kisanaa. Naye Senkoro (1988: 15) anaeleza taswira, katika ushairi, kuwa maneno yalivyopangwa katika shairi huweza kuchora picha kamili ya kitu, hali, wazo, dhana au uzoefu fulani wa jamii au sehemu ya jamii katika mawazo ya wanaopokea shairi linalohusika. Senkoro anaendelea kueleza kuwa matumizi ya taswira mara nyingi huambatana na yale ya ishara ambazo nazo aghalabu hufichwa ndani ya tamathali za semi. Pia, anaendelea kuifasili ishara kuwa ni dhana au mawazo mbalimbali anayotumia msanii katika kazi yake ya fasihi kuwakilisha vitu, dhana au mawazo mengine. Aidha, Mulokozi na Kahigi (1979: 28) wanaeleza kuwa picha ni matumizi ya lugha yanayopambanuliwa na uteuzi mzuri wa maneno, uangalifu na udhahiri wa maelezo yenye kuhusisha na kujumuisha dhana mbalimbali tofauti ndani ya dhana moja ili kuleta taswira na athari maalumu katika mawazo ya msomaji (au msikilizaji). Hata hivyo, kiwakilisho hicho anachokielezea Msokile (1992) sio cha maneno au hisi tu bali pia kinaweza kuwa cha matendo, hasa katika kazi za fasihi simulizi kama vile katika nyimbo na ngonjera. Vilevile zipo picha za maumbile. Picha hizi zinaweza

kutafsiriwa na msomaji au msikilizaji kwa maana mbalimbali kutokana na uzoefu na ufahamu wake.

Nyimbo za uganga wa pepo katika makala hii pia zimetumia lugha ya picha na ishara ili kuleta mvuto na kulielezea jambo au hali fulani kisanaa na kuwawezesha wasomaji au wasikilizaji kupata hisi juu ya jambo au hali fulani. Pia, mbinu ya picha imesaidia kuficha kile kilichokusudiwa na mwimbaji kwa kuwa mara nyingi hutumika pamoja na ishara. Picha na ishara ni sharti zitafsiriwe na zifasiliwe ili kupatikana maana ya kile kilichokusudiwa na msanii. Maana ya picha inayopatikana ni ya hisi; hisi hizi zinaweza kuwa za kusikia, kuona, kuonja, kunusa na kugusa. Kama wasemavyo Mulokozi na Kahigi (1979) na Msokile (1992) kuwa matumizi ya picha yanaweza kumfanya msomaji au msikilizaji wa kazi ya fasihi asisimke, aogope, afurahike, avutike, akirihishwe, alie, anyamae, aghadhibike, acheke na anune kwa kuathiriwa na picha zilizoteuliwa na kusanifiwa kwa ufundi. Hali zote hizi, msomaji au msikilizaji huzipata kutokana na hisi anazozipata kupitia viungo vyake vya hisia. Kuficha ni moja ya sifa za fasihi.
Katika muktadha wa kiganga, picha hujitokeza zaidi wakati wa kufanya uganga wenyewe kwani, mara nyingine nyimbo hizi za uganga zinapoimbwa huambatana na matendo ambayo huwa ni ishara ya tabia fulani. Ishara hizo ndizo zinazotoa picha ya hisi. Kwa mfano, katika utafiti huu wakati wimbo ‘Tuvute Mkasia’ ulipoimbwa mwari-mpungwa /muwele alikamatwa mikono kwa mbele na mwari mkubwa (mtu aliyepungwa zamani) huku akivutwa mbele na nyuma kama mtu anayepiga makasia katika ngalawa. Hii ni ishara lakini pia inajenga picha ya namna mtu anavyopiga makasia katika chombo cha baharini. Katika muktadha wa uganga wimbo huu unaashiria kuwa wapo majini/pepo wanaokaa baharini kwa hiyo akiimbiwa wimbo huu hufurahi sana na huja haraka katika kichwa cha muwele. Maneno ya wimbo huo ni kama ifuatavyo:

| **Wimbo katika Kitumbatu**<br>**Tuvute Mkasia**<br>(wimbo wa kuhamasisha pepo aje haraka) | **Tafsiri kwa Kiswahili**<br>**Tuvute Makasia** |
|---|---|
| 1. *Tuvute mkasia, kimaua x2* | 1. Tuvute makasia, kimaua x2 |
| 2. *Ooh mkasia* | 2. Ooh makasia, |
| 3. *Kimaua majini yasonga,* | 3. Kimaua majini yanasogea, |
| 4. *Yanakuja.* | 4. Yanakuja. |
| 5. *Hayo hayo, yanakuja.* | *5.* Hayo hayo, yanakuja. |

Aidha, katika wimbo ‘Nyumba ya Bati’ (wimbo wa kuhamasisha pepo aje haraka) tunapata picha ya nyumba ya bati inayovuja mtwiko. Kwa kawaida nyumba iliyoezekwa kwa bati haitarajiwi kuvuja lakini nyumba hii ya mganga inavuja na ndio anasema, ‘naona ajabu nyumba ya bati kuvuja mtwiko’. Nyumba iliyoezekwa kwa makuti ndiyo inayotarajiwa kuvuja mtwiko. BAKIZA (2010: 283) wanaeleza

kuwa mtwiko ni mwamba wa juu kabisa unaokutanisha mapaa ya nyumba au ni mfuniko unaofunika uwazi kwenye kingo zilipokutana bati au makuti yaliyoezekwa. Hapa tunapata picha ya nyumba iliyoezekwa kwa bati lakini ikinyesha mvua inavuja mtwikoni, jambo ambalo si la kawaida kwa nyuma ya aina hii. Wimbo huo unasema:

*Kichaka kiko x2*
*Naona ajabu nyumba ya bati kuvuja mtwiko*.

Ishara inayopatikana hapa ni ya matatizo aliyonayo mtu mzima aliyekuwa ameshaezeka bati. Kuezeka bati ni msemo wenye maana ya kuwa na mvi (rangi ya mvi inafananishwa na bati kwa kuwa aghalabu bati ni nyeupe). Na mvi kwa Waswahili ni busara na hekima. Kuvuja mtwiko kunaashiria kuwa na matatizo ambapo haikutarajiwa kwa mtu kama huyo kuwa na matatizo na kushindwa kuyatatua badala yake anatafuta waganga wengine kumtatulia na ndiyo maana mwimbaji anaona ajabu. Kwa hivyo, hapa msomaji au msikilizaji wa wimbo huu anapata hisi ya kuona ambayo inamfanya atoe maana kama hiyo iliyoelezwa hapo juu.

Matumizi mengine ya ishara yanapatikana katika wimbo ‘Jini Jaburani’ (wimbo wa kuchombezea pepo aje kichwani mwa muwele). Katika wimbo huu kuna matumizi ya neno *maua* kuashiria watoto au mwari-mpungwa, na *ndege* kuashiria watu wabaya wanaokula maua. Hivyo Jini Jaburani anaambiwa aende akawalinde watoto/mwari- mpungwa kwa sababu wanadhuriwa na watu wabaya. Aidha, katika wimbo huu inachorwa picha ya ndege anayekula maua na kwamba jini Jaburani anaombwa aende kuwafukuza hao ndege (watu wabaya). Maneno ya wimbo huo ni kama yafuatayo:

1. *Jini Jaburani ondoka ukawinge*
2. ***Maua** yanaliwa na **ndege**.*

Mfano mwingine wa ishara unajitokeza katika wimbo ‘Nyuki’ (tulishauelezea hapo juu) ambapo mtunzi anatumia maneno *jiwe la msio*. Jiwe la msio ni jiwe maalumu lililotengenezwa kwa ajili ya kusagia liwa (unga unaotokana na mti wa msandali) unaotumiwa na wanawake kujipaka ili kuondoa vipele na kusafisha ngozi ili wapendeze. Aidha, liwa hutumiwa na akinamama kwa ajili ya kusingia (kusugua mwili kwa kutumia liwa). Kwa hivyo, *jiwe la msio* limetumiwa kama ishara ya urembo kwa wanawake kwa kuwa ndilo wanalotumia kutengenezea dawa ya kujiremba, liwa. Kwa mila za Wanzanzibari, jiwe hili la msio haliwekwi ovyoovyo; huhifadhiwa ndani ya nyumba na liwa husagwa nyumbani, sio hadharani. Kwa maana hiyo, kulikanyaga jiwe la msio kama ilivyoelezwa katika wimbo ni utovu wa adabu na kuwadharau wanawake na ndiyo maana nyuki (watu) wanakwenda mbio kukimbia utovu huo wa adabu na kwamba hawakubaliani na tabia hiyo. Kwa mantiki hiyo, kukanyaga jiwe la msio ni uchokozi. Katika

muktadha wa kiganga nyuki ni ishara ya waganga ambao baada ya kumpunga mwari kwa muda mrefu bila ya mafanikio huonekana wakikimbia kwenda huku na huko kumtafuta pepo na ndipo wimbo huu huimbwa kwani mwari huyo hakupaswa kupungwa/kutibiwa kwa kuwa maradhi yake yamesababishwa na binadamu, sio Mola. Hali hii ya pepo kutopanda kichwani mwa muwele haraka inasababishwa na mtu mbaya kwa makusudi ili kuwataabisha kumtafuta pepo huyo. Aidha, tunachorewa picha ya nyuki wanaokwenda mbio huku na huko kama ilivyoelezwa.

## 2.5 Matumizi ya Misemo

Misemo mbalimbali pia imetumika katika utunzi wa nyimbo hizi. Misemo katika nyimbo hizi za uganga wa pepo, pamoja na mambo mengine, hutumika kuficha kinachokusudiwa na mtunzi. BAKIZA (2010: 271) wanaeleza kuwa msemo ni tungo yenye maana maalumu ambayo ni tofauti na ile ya kawaida isiyolinganisha hali mbili. Pia, tunaongezea kwamba msemo ni tungo ya kisanaa na maana yake inategemea jamii na mazingira inamotumiwa. Sio kila mtu anaweza kujua maana ya kila msemo. Pia, misemo ina dhima ya kupamba mazungumzo na maandishi ili kumfanya msikilizaji au msomaji avutiwe na asichoshwe na mazungumzo. Mathalani, Masebo na Nyangwine (2002) wanaeleza kuwa misemo hutumiwa kwa ajili ya kupamba lugha na kutajirisha maelezo ya wahusika. Kuna misemo ya aina nyingi kutegemea mazingira na muktadha inamotumika. Kwa mfano, kuna misemo ya kivuvi kama *heri ya damani*; ya kimichezo kama *michezo ni afya*; ya kilimo kama *kilimo cha kufa na kupona*; ya tiba kama *afya njema ni silaha*; ya kielimu kama *elimu ni ufunguo wa maisha,* na ya kiganga. Kwa hivyo, misemo ni kipera cha semi. Misemo hii ina maana na dhima maalumu katika maandishi, mazungumzo au fasihi kama vile katika nyimbo. Mathalani, katika wimbo wa 'Bamba' (wimbo wa kumalizia uganga wa puuwo) msemo *bamba la mvumo* umetumika kumaanisha ubaya (pepo) aliopewa mtu ambao umemuathiri na bado unaendelea kumuathiri. Kutokana na tanzu na vipera vya fasihi simulizi kuingiliana tunagundua kuwa msemo huu pia ni fumbo; wanafumbwa wenye mgonjwa na wakati huohuo ni ishara ya ubaya aliofanyiwa mgonjwa. Wimbo huo unasema:

| **Wimbo katika Kitumbatu** | **Tafsiri kwa Kiswahili** |
|---|---|
| 1. *Bamba la mvumo x2,* | 1. Bamba la mvumo x2, |
| 2. *Limenichoma kidole,* | 2. Limenichoma kidole, |
| 3. *Bado liwa mumo,* | 3. Bado limo mumo, (bado limeganda) |
| 4. *Bamba la mvumo.* | 4. Bamba la mvumo. |

Misemo mingine imetumika katika wimbo 'Ng'oa Nanga' (wimbo wa kumalizia uganga wa maruhani), ambapo *kung'oa nanga* humaanisha kuondoka na *kutweka*

humaanisha kuanza kufanya jambo. Hii ni misemo ya watu wa pwani. Mtu ambaye si wa mazingira hayo si rahisi kujua maana yake, kwani kutweka ni kitendo cha kupandisha tanga juu ya mlingoti wakati chombo kinapotaka kuondoka; na kung’oa nanga ni kitendo cha kupandisha nanga na kuitia chomboni ili kuanza safari. Misemo hii inajitokeza katika wimbo huo kama ifuatavyo:

| **Wimbo katika Kitumbatu** | **Tafsiri kwa Kiswahili** |
|---|---|
| 1. ***Tunang’oa nanga*** *ee x2,* | 1. Tunaondoka ee x2, |
| 2. *Tungoje usiku uche.* | 2. Tusubiri usiku uche. |
| 3. *Kijogoro cha Makungu,* | 3. Kijogoo cha Makungu, |
| 4. *Kinangoja Zabibu* ***atweke****.* | 4. Kinasubiri Zabibu aanze, |
| 5. *Tunang’oa nanga wee ee,* | 5. Tunaondoka wee ee, |
| 6. *Tungoje usiku uche.* | 6. Tusubiri usiku uche. |

Halikadhalika, katika wimbo ‘Sina Hailipi Deni’ (wimbo wa maruhani ambao huimbwa pepo anapolipwa kilemba au chano) (wimbo huu tayari tulishaurejelea hapo awali) kuna matumizi ya msemo *sina hailipi deni* ukiwa na maana ya kutochukua hatua yoyote au kutofanya bidii katika kufanya jambo au kusuluhisha tatizo. Ili usiwe na deni ni vema ulipe, si vinginevyo. *Kuvuta mkasia* pia ni msemo uliotumiwa kumaanisha kuchangamkia au kufanya jambo kwa bidii. Vilevile, kuvuta mkasia katika wimbo wa uganga wa pepo ni kumkamata mwari/muwele mikono kwa mbele huku ukimpeleka mbele na nyuma kwa kasi ili kumfanya shetani/pepo apande kichwani haraka. Katika muktadha wa kiganga, msemo huu umetumika kama fumbo kwa watu wenye mgonjwa apungwaye kwamba walikaa muda mrefu bila ya kumlipa pepo waliyemuahidi siku ya mwanzo mgonjwa wao alipopungwa. Mtu apungwaye mara nyingi hutakiwa amlipe pepo chano (vyakula) au mnyama kama mbuzi lakini watu wengine hawatimizi miadi, hivyo hupitiliza siku walizoahidiana kulipa. Na hapo ndipo pepo huanza tena kumsibu mtu yule aliyewahi kupungwa. Wanapoamua kumlipa ndipo siku ya uganga waganga huutumia msemo huu katika wimbo kwamba sina hailipi deni. Na usipolipa deni (usipotatua matatizo) yataendelea kubakia.

## 2.6 Matumizi ya Tamathali za Semi

Tamatahali za semi ni fungu la maneno lililogeuzwa maana yake kamili ili kuwasilisha maana nyingine (Madumulla, 2009: 146). Nao Mulokozi na Kahigi (1979: 32) wanafasili tamathali za semi kuwa ni vifananisho au viwakilisho vya dhana nyingine tofauti au zinazofanana. Ni usemi wenye kupanua, kupuuza au kubadilisha maana za dhahiri au za kawaida za maneno ili kuleta maana maalumu ya kishairi iliyokusudiwa na mtunzi. Kwa ujumla wataalamu hao wanaeleza kuwa tamathali za semi ni semi za kisanaa ambazo humithilisha au hufananisha vitu viwili au hali mbili zenye sifa na tabia zisizofanana moja kwa moja. Madumulla

anazigawa tamathali za semi katika makundi makuu matatu: i) tamathali za mlinganisho kama vile sitiari, tashbiha, tashihisi na taashira, ii) tamathali za mafumbo kama vile dhihaka, tasfida na shitihizai, na iii) tamathali za msisitizo kama vile mubaalagha na ritifaa. Hata hivyo, katika nyimbo za uganga zilizokusanywa katika utafiti huu, tamathali za semi hazikutumika sana; tamathali iliyojitokeza zaidi ni tashihisi. Tashihisi ni aina ya tamathali ya semi ambayo hutumika katika kazi ya fasihi kutia uhai kitu kisicho na uhai au kikipa sifa na tabia ya utu (Mdungi, 2016: 91). Nao Masebo na Nyangwine (2002: 54) wanafasili tashihisi kuwa ni tamathali ambazo vitu hupewa uwezo wa kutenda kama mtu. Kwa hivyo, kwa ufupi, tashihisi ni tamathali ya semi ambapo vitu visivyo na sifa au tabia ya kutenda matendo kama afanyavyo binadamu hupewa uwezo huo. Mathalani, katika wimbo wa ‘Sina Hailipi Deni’ (tuliokwishaurejelea hapo awali), neno ‘sina’ linapewa uwezo wa kiutu, kutolipa deni. Pia, katika wimbo wa ‘Kombo’ (wimbo wa maruhani wa kuanzia uganga) tashihisi zimetumika kama ifuatavyo:

| **Wimbo katika Kitumbatu** | **Tafsiri kwa Kiswahili** |
|---|---|
| 1. *Kombo wee! wenda wapi na kilio?* | 1. Kombo wee! Unakwenda wapi na kilio? |
| 2. ***Maharagwe yavunju ukaango**, na **mwiko ukenda mbio.*** | 2. Maharagwe yamevunja ukaango na mwiko ukaenda mbio |
| 3. *Kombo wee, wenda wapi na kilio?* | 3. Kombo wee unakwenda wapi na kilio? |

Katika wimbo huu *maharagwe* na *mwiko* vinapewa urazini; maharagwe yanapewa uwezo wa kuvunja ukaango na mwiko nao unapewa uwezo wa kwenda mbio kama afanyavyo binadamu. Pia, kuna matumizi ya tashbiha katika wimbo wa uganga wa puuwo uitwao ‘Lemba’ ambapo katika mstari usemao *lemba langu linang’ara kama ngao*, ung’araji wa kilemba unalinganishwa na ule wa ngao. Hii ina maana kuwa kilemba anachopewa muwele ni kizuri sana. Wimbo wote huu umeundwa kwa tashbiha kwani una huo mshororo mmoja tu.

## 3.0 Hitimisho

Katika makala hii tumejadili mbinu za utungaji wa nyimbo za uganga wa pepo kama unavyofanywa katika Mkoa wa Kaskazini Unguja, Zanzibar. Tumegundua kuwa katika nyimbo hizi watunzi/wasanii hutunga nyimbo zao ama kwa kufuata urari wa vina na mizani au kwa kutofuata kaida hizo. Zile zinazofuata kaida ya kutumia vina, basi nyingi zina vina vya mwisho kutokana na maumbo yao kuwa madogo ambayo husababisha *tempo* (mwondoko) zao kuwa za harakaharaka. Nyimbo hizi kwa kiasi kikubwa hutumia mbinu ya kuficha yale yaliyokusudiwa na msanii, hivyo zinatumia lugha ya picha na ishara na misemo mbalimbali ya kiganga. Vilevile wasanii wake wanatumia maneno yenye asili ya lahaja ya Kitumbatu au Kipemba kutokana ama na asili ya uganga au lahaja ya mwimbaji

wa nyimbo hizo. Maneno yenye asili ya dini ya Kiislamu na lugha ya Kiarabu pia hutumika hususani katika uganga wa maruhani (komero) kwani inaaminika kuwa maruhani ni pepo/jini mwenye asili ya Uarabuni na pia wapo waumini wa dini ya Kiislamu.

Kwa hakika uwanja huu wa nyimbo za uganga wa pepo hapa Tanzania haujashughulikiwa sana; kwa hivyo, inafaa wataalamu na wapenzi wa fasihi na utamaduni wa Kiswahili kufanya utafiti zaidi katika uga huu ili kuhifadhi yatokanayo. Tafiti nyingi zilizowahi kufanywa ni zile za kianthropolojia – zinajadili zaidi uganga wenyewe unavyofanywa na malengo yake kwa jamii ya Waswahili. Kwa mfano, Giles (1987) anasema kuna pepo au majini wa aina mbili: Waislamu na washenzi. Pia, anaeleza kuwa shetani, jini au pepo anaweza kuwa Muislamu (mzuri/mwema) na mshenzi (mbaya). Pepo wazuri hutumiwa kuwalinda na kuwasaidia watu katika maisha yao ya kila siku na wale wabaya ndio wanawadhuru watu.

## Marejeleo

Abedi, K. A. (1954). *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Alpers, E. A. (1984). "Ordinary Household Chores: Ritual and Power in a 19$^{TH}$ –Century Swahili

Women's Spirit Possession Cult", International *Journal of African Historical Studies*, 17 (4), kur. 683-684.

BAKIZA (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Nairobi: Oxford University Press.

________ (2008). *Utamaduni wa Mzanzibari.* Zanzibar: BAKIZA. Kur. 63-67.

Mdungi, A. M.(2016). "Matumizi ya Tamathali za Semi na Vipengele vyengine vya Lugha Baina ya Muyaka wa Muhaji na Shaaban Robert". Jahazi, Zanzibar: BAKIZA. kur.87-88.

Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Africa*. Nairobi: Oxford University Press.

Giles, L. (1987). "Possession Cults on the Swahili Coast: A Re-Examination of Theories of Marginality", Africa, 57 (2). kur. 240-241.

Haji, H. G. (2011). "Mitindo ya Nyimbo za Uganga wa Pepo". Tasnifu ya Digrii ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dodoma. (Haijachapishwa).

Madumulla, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili*. Nairobi: Mture Educational Publishers Limited.

Masebo, J. A. na Nyangwine, N. (2002). *Kiswahili Kidato cha 3 & 4: Historia, Fasihi, Sarufi, Matumizi, Utungaji na Ufahamu.* Dar es Salaam: Afroplus Industries Ltd.

Msokile, M. (1992). *Misingi ya Hadithi Fupi.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Mulokozi, M.M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mulokozi, M. M. na Kahigi, K. K. (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu.* Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Nkwera, F. V. (h.t.). *Tamrini za Fasihi Simulizi*. Dar es Salaam: Business Printers Limited.

Rashid, A. M. (2008). “Namna ya Kutunga Bahari mbalimbali za Ushairi wa Kiswahili”, *Utamaduni wa Mzanzibari*. Zanzibar: BAKIZA. kur. 66-67.

Senkoro, F. E. M. (1988). *Ushairi: Nadharia na Tahakiki*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.